

Jinsi ya Kufanya Kipimo cha COVID-19


Kwa kutumia Kipimo nyumbani cha *QuickVue At-Home OTC COVID-19*

KUHUSU

Huu ni muongozo uliorahisishwa kwa ajili ya seti ya kipimo cha *QuickVue At-Home OTC COVID-19*. Kwa taarifa kamili, tafadhali rudia katika karatasi ya Muongozo pamoja na **Patient Fact Sheet (Karatasi ya Kueleza Ukweli ya mgonjwa)** ndani ya seti. Bidhaa hii imeidhinishwa na FDA kwa Matumizi ya dharura.



Kwa video inayohusu jinsi ya kufanya kipimo, tembelea quickvueathome.com/#video_testkit-2



NINI ZAIDI UNACHOHITAJI?

Saa au kipima muda (Haikujumuishwa)
Kuwa sahihi kuhusu muda ni muhimu sana kwa kipimo hiki!




KUANZA KUPIMO

Osha mikono yako na weka seti juu ya sehemu safi na iliyo sawasawa. Hakikisha kuna mwanga mzuri ndani ya chumba. Endapo unamfanyia kipimo mtu mwingine vaa Barakoa. Fungua seti na hakikisha kuwa vitu vyote viliorodheshwa juu vinapatikana. Chukua saa yako au kipima muda chako na fuata muongozo hatua kwa hatua kutoka upande mwingine wa karatasi.

Kufanya Kipimo

1


Ondoa kifuniko kutoka moja ya bomba na weka ndani ya kishikizi bomba



USIGUSE KICHWA CHA USUFI


2

Chambua wazi kizengeresha kutoka kwenye usufi. Usiguse kichwa cha usufi




3

Ingiza usufi kwa inchi ½ hadi ¾ ndani ya tundu moja la pua na sugua kwa kuzungusha kwenye kuta za ndani kwa angalau mara 4. Ukitumia usufi huohuo, rudia kwenye tundu la pua jengine. Hii itachukua sekunde 15.



4

Mara baada ya kupata sampuli kutoka puani, weka usufi ndani ya bomba iliyowazi. Hakikisha kuwa usufi unagusa chini ya bomba. Koroga usufi mara 3 au 4



5


Acha usufi ndani ya bomba kwa **angalau dakika 1**. (Tumia saa au kipima muda!) Matokeo yasiyo sahihi yanaweza kutokea endapo utaacha usufi ndani kwa muda mfupi au kwa muda mrefu.



Acha usufi ndani kwa angalau dakika 1!

6

Baada ya dakika 1, toa usufi kutoka kwenye bomba, **sugua kichwa cha usufi katika kuta za bomba** ili kupunguza majimaji kadri ya iwezekanavyo. Tupa usufi.




7

Fungua mfuko wa mstari wa kipimo kwa uangalifu na weka mstari wa kipimo ndani ya bomba lililowazi huku **mishale ikiashiria chini**. Acha mstari huo ndani ya bomba kwa **dakika 10**. (Tumia saa au kipima muda!)



Acha msitari wa kipimo ndani kwa angalau dakika 10.



Mishale inaashiria chini

8

Baada ya dakika 10, toa mistari ya kipimo nje ya bomba na weka sehemu iliyo sawa yenye mwanga mzuri. **Soma mstari wa kupimo haraka!** Endapo utasubiri zaidi ya dakika 5 kusoma, unaweza pata majibu yasiyo sahihi au batili.



Kusoma Majibu Yako ya Kipimo

Kuna aina 3 za majibu ya kipimo yanayawezekana: **Chanya**, **Hasi** au **Batili**, kipimo ambacho hakiwezi kutumika



MATOKEO CHANYA =
Msitari wa pinki 1 + Msitari wa bluu 1

Inawezakana ukawa na COVID-19. **Unapaswa kujitenga**. Endapo una dalili ambazo zinakusumbua au kukupa wasiwasi, wasiliana na mtoa huduma wako wa afya.



MATOKEA HASI =
Msitari wa bluu 1

Inawezakana kuwa hauna COVID-19. Lakini endapo una dalili ambazo zinakusumbua au kukupa wasiwasi, wasiliana na mtoa huduma wako wa afya.



MATOKEO BATILI =
Msitari wa pinki 1 au HAKUNA misitari

Utahitaji **kufanya kipimo kipya**. Anza tena kuanzia mwanzo kwa kutumia bomba mpya, usufi, na mistari ya kipimo. Kwa matokeo batili mawili (2), piga 1-833-784-2588.